



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



SIMU NA 0737235630

Email- ded.itigidc@singida.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HW/ITG/S.1/22 VOL III/82

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi
01 Barabara ya Halmashauri
S.L.P 70,
43483 ITIGI - SINGIDA.

16 Oktoba, 2023.

WANANCHI WOTE,
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI.

Kuh: **TANGAZO LA KAZI ZA MKATABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote wenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi 41 za ajira ya mkataba kwa kazi ya **Wakusanya Mapato na Walinzi**.

2. Kwa mujibu wa miundo ya Utumishi wa Umma kazi zinazotangazwa ni:-

1. **WAKUSANYA MAPATO NAFASI 29**

a) **SIFA ZA KUINGILIA**

a) Awe raia wa Tanzania

ii) Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi na vyeti vyake viwe halali visivyo na shaka yoyote.

iii) Awe na umri wa kuanzia miaka 18 – 45

iv) Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

b) **MAJUKUMU YA MKUSANYA MAPATO**

a) Kukusanya ushuru kwa kutumia mashine za Kielektroniki (POS)

ii) Kuhakikisha anapeleka Benki au Halmashauri mapato aliyokusanya kwa kila siku

iii) Iwe angalizo la upotevu/uchakavu wa mashine

- iv) Kuwasilisha Halmashauri Hati ya kuingiza fedha benki kwa akaunti ya Halmashauri (Pay Slip).

c) UTARATIBU WA MALIPO

Mkusanya mapato (MM) wa ajira ya Mkataba atalipwa kulingana na mkataba atakaolingia na Halmashauri wa makusanyo atakayokusanya na kuyapeleka benki kila mwezi.

2. WALINZI NAFASI 12

i) SIFA ZA KUINGILIA

- a) Awe raia wa Tanzania
- b) Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi na vyeti vyake viwe halali visivyo na shaka yoyote.
- c) Awe amefuzu mafunzo ya mgambo/Polisi/JKT au mafunzo ya zimamoto kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali
- d) Awe na umri kuanzia miaka 18-45
- e) Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

ii) MAJUKUMU YA MLINZI AU MGAMBO

- a) Kulinda na kuimarisha usalama katika mageti yanayotumika katika ukusanyaji wa mapato
- b) Kusimamia, kuboresha na kuimarisha vizuizi vyote vya kukusanya mapato kwenye vituo atakapopangiwa kufanya kazi
- c) Kutoa ushauri wa jinsi ya kuboresha huduma ya ulinzi katika geti analolinda (mahali pa kazi)

d) UTARATIBU WA MALIPO

Mlinzi/Mgambo wa ajira ya mkataba atalipwa kulingana na mkataba atakaolingia na Halmashauri wa makusanyo yatakayokusanywa na kupeleka benki na mkusanya mapato kwa kila mwezi

3. MASHARTI YA AJIRA KWA UJUMLA

- a) Ajira hizi ni za Mkataba ambayo itazingatiwa kulingana na masharti yaliyowekwa katika makubaliano.

- b) Mwongozo anatakiwa awe na mdhamini mwenye mali isiyohamishika yenye thamani isiyopungua **TSHS. 3,000,000** ambapo mdhamini huyo atatakiwa kusaini Mkataba wa udhamini kama mwombaji atapata kazi aliyoomba.
- c) Mwombaji wa kazi ya mkusanya mapato au mlinzi awe tayari kufanya kazi sehemu yeyote atakayopangiwa katika mageti ya Mwamagembe, Rungwa, Aghondi, Maliasili, Mizani, Sanjaranda, Idodyandole, Doroto, Njirii, Itigi Majengo, Itigi Mjini, Tambukareli, Kitaraka na Mitundu.
- d) Mwombaji ambaye alishawahi kufanya kazi ya ukusanyaji wa mapato na ana deni haruhusiwi kuomba mpaka pale atakapomaliza kulipa deni lote.

4. AINA YA AJIRA

Ajira itakuwa ni ya Mkataba wa miezi mitatu (3) kuanzia kila mwombaji atakapokamilisha vigezo kwenye sifa za kuingilia na masharti ya ajira katika kila nafasi iliyotangazwa.

5. NYARAKA ZA KUAMBATISHA KATIKA BARUA YA MAOMBI

- i) Taarifa binafsi (CV)
 - ii) Nakala ya vyeti vya elimu na mafunzo
 - iii) Cheti cha kuzaliwa
 - iv) Mawasiliano (namba za simu)
 - v) Picha 2 za rangi (Passport size)
6. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **22/10/2023** saa tisa na nusu (**9:30**) alasiri.

7. MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi,
S.L.P 70,
ITIGI.

8. TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:

John K. Mgalula
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**